WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

KIKAO CHA KAMATI YA AFYA YA MSINGI, MPWAPWA.

SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI NA CHANJO YA KUZUIA SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI (HPV VACCINE)

Utangulizi

- Saratani – mabadiliko ya ukuaji wa seli au chembechembe hai na yaweza tokea sehemu yoyote ya mwili (seli hukua na kuongezeka idadi kwa haraka sana).
- Saratani ya mlango wa kizazi (cervix) ni mabadiliko ya ukuaji wa seli za mlango wa kizazi.
- Saratani hii inaweza kusambaa na kuweza kushambulia kibofu cha mkojo, uke na sehemu ya chini ya utumbo mkubwa na baadaye figo, ini na sehemu zingine za mwili na kusababisha kifo.
- Kwa Tanzania hii ndiyo saratani inayoongoza kusababisha vifo kwa wanawake wengi kwa sababu asilimia 70 huripoti wakiwa wamechelewa sana

ORCI NEW CANCER CASE DISTRIBUTION, 2006-2016

TYPE of Cancer	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
Cervical cancer (Mlango wa kizazi)	955	1006	1288	1374	1510	1881	1896	1795	1867	1892	1934
Breast cancer (kansa ya matiti)	244	245	275	322	386	526	667	705	733	742	758
Kaposis Sarcoma	295	404	418	447	681	814	789	654	680	674	689
Esophageal ca (kansa ya koo)	221	256	282	307	380	511	573	601	625	643	657
Head & Neck (kicha na shingo)	155	206	244	272	289	361	386	411	427	439	449
Lymphomas (Kansa ya tezi)	201	199	226	245	186	269	295	295	307	314	321
Leukemias (kansa ya damu)	56	78	87	103	142	261	252	251	269	253	259
Urinary Bladder (kansa Kibofu)	56	88	87	98	109	153	168	168	175	182	186
Skin (kansa ya ngozi)	50	108	111	123	129	141	147	147	153	161	165
Eye (Kansa ya Jicho)	46	76	80	95	84	119	131	134	139	143	146
Prostate (tezi dume)	51	69	75	85	96	93	101	116	121	129	132
Other	467	403	69	305	203	115	124	179	186	192	196
Total	2807	3138	3480	3776	4195	5244	5564	5464	5683	5764	5891

Nini kinasababisha ugonjwa wa saratani?

- Karibu saratani zote za mlango wa kizazi husababishwa na virusi vya Human Papilloma.
- Kuna aina zaidi ya 40 ya virusi vya Human Papilloma vinavyoweza kusababisha maambukizi kwenye njia za uzazi za wanawake na wanaume, mdomoni na kwenye koo.
- Virusi vya HPV aina ya 16 na 18 ndio vimethibitika kusababisha asimia kubwa ya saratani zote za mlango wa kizazi duniani
- Maambukizi ya virusi hivi huwa hayaonyeshi dalili zozote na kwa watu wengi. Asilimia 10 hadi 20 ndio huja kupata dalili za saratani miaka 10 hadi 30 baadae.

Visababishi vya maambukizi ya virusi

- Kuanza kujamiana katika umri mdogo
- Kuwa na wapenzi wengi
- Kuwa na ndoa za mitala
- Kuzaa watoto wengi
- Uvutaji sigara

Dalili za saratani ya mlango wa kizazi

- Kutokwa damu bila mpangilio au kutokwa damu baada ya kujamiana
- Maumivu ya mgongo, miguu na au kiuno
- Kuchoka, kupungua uzito, kupungikiwa hamu ya kula
- Kutokwa uchafu uchafu kwenye uke wa majimaji, uliopauka wa rangi kahawia au wenye damu
- Kuvimba mguu mmoja

Dalili za saratani ya mlango wa kizazi

Dalili mbaya zaidi zinazoweza kujitokeza ni pamoja na:

- Kuishiwa damu
- Figo kushindwa kufanya kazi
- Kupatwa na fistula, na uvimbe wa tezi

Kinga ya saratani ya mlango wa kizazi

- Kinga ya awali ni pamoja na:
  - Kupata chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi (HPV vaccine),
  - Kubadili tabia,
  - Kuepuka ngono katika umri mdogo,
  - Kuepuka uvutaji wa sigara,
  - Kuepuka kubeba mimba katika umri mdogo na kuwa na mwenzi mmoja mwaminifu.
- Kinga kwenye **hatua za mwanzo** ni kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kubaini dalili za mwanzo na kupata matibabu stahiki. (cervical cancer screening)

CHANJO YA HPV

- Chanjo ya HPV ni kinga dhidi ya virusi vya HPV vinavyosababisha saratani ya mlango wa kizazi
- Chanjo hii ina kinga wanawake dhidi ya maambukizi ya virusi vya HPV vinavyosababisha saratani ya mlango wa kizazi
- Chanjo hii inakinga virusi aina ya 6,11,16,18 vinavyosababisha saratani ya mlango wa kizazi.
- Chanjo ya HPV ni salama imethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)
- Chanjo ya HPV ni kinga na sio tiba ya saratani ya mlango wa uzazi.

Umri unostahili kupata chanjo ya HPV

- Chanjo ya HPV inatolewa kwa wasichana wenye umri wa miaka 9 - 14.

- Kwa mwaka 2018, chanjo hii itatolewa tu kwa wasichana wanapotimiza umri wa miaka 14.

- Wasichana hawa ni wale wote waliozaliwa kuanzia 01 Januari hadi 31 Disemba 2004.

Ratiba ya utoaji wa chanjo ya HPV

- Chanjo hii inatolewa mara mbili ili kupata kinga kamili.

- Baada ya kutoa chanjo (dozi) ya kwanza, chanjo (dozi) ya pili inatakiwa kutolewa ***baada ya miezi sita.*** (0, 6)

- Ikiwa mlengwa (msichana) amechelewa kupata dozi ya pili, anaweza kupewa dozi hiyo ***ndani ya muda wa miezi 12 baada ya dozi ya kwanza***

UHAMASISHAJI

- Uanzishwaji wa chanjo ya HPV kwa wasichana walengwa utakuwa na mafanikio iwapo mawasiliano na uhamasishaji wa jamii utafanyika kikamilifu
- Uhamasishaji inabidi **ufanyike kabla**, **wakati** na **baada** ya uanzishwaji wa chanjo ya HPV
- Wadau wote kutoka katika jamii washirikishwe kikamilifu katika nyakati mbalimbali na muda muafaka kuelekea kwenye uzinduzi
- Aidha, maongezi ya ana kwa ana yanasaidia kwa kiasi kikubwa kumshawishi mzazi/mlezi au mlengwa kupata huduma za chanjo ya HPV

Ujumbe muhimu kwa jamii

- Chanjo ya HPV huwakinga wasichana wasipate saratani ya mlango wa kizazi pindi wawapo watu wazima
- Saratani ya mlango wa kizazi huathiri via vya uzazi kwa wanawake na ndiyo inayoongoza kusababisha vifo kwa wanawake wenye uwezo wa kushika ujauzito.
- Wasichana hawana budi kupata chanjo ya HPV wakiwa wana umri mdogo kabla ya kuambukizwa
- Unaweza kumkinga binti yako sasa na maisha yake ya baadae kwa kuhakikisha kuwa anapata chanjo ya kukinga saratani ya mlango wa kizazi (*HPV vaccine*)

Ujumbe muhimu kwa jamii

- Chanjo ya HPV ni salama, haina madhara na haiathiri uwezo wa binti kupata watoto hapo baadae.
- Chanjo ya HPV inatolewa bila malipo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya, shuleni na kwenye vituo vya huduma za mkoba.
- Ili kupata kinga kamili, binti anatakiwa apate chanjo ya HPV mara mbili. Chanjo ya pili anatakiwa aipate miezi sita baada ya kupata chanjo ya kwanza.
- Serikali imekubali usalama na umadhubuti wa chanjo ya HPV katika kukinga saratani ya mlango wa kizazi, ndio maana imeamua kuianzisha ili iweze kusaidia kudhibiti tatizo hili hapa nchini.

WIKI YA CHANJO AFRIKA

- Tanzania imechagua chanjo hii ianze kutolewa wakati wowote kuanzia tarehe 23-29 April 2018, wakati shirika la Afya Duniani – eneo la AFRIKA (WHO African Region) tunasherehekea wiki ya chanjo (African Vaccination week –AVW
- Nia ni kutoa hamasa kuhusu umuhimu na haki ya kila mtu haswa watoto na wanawake kulindwa kutokana na magonjwa yale yanayokingwa kwa kupatiwa chanjo
- Chanjo nyingine ya ziada ya kulinda ugonjwa wa kupooza (Inactivated Polio Vaccine) itaanza kutolewa

Asanteni kwa kunisikiliza